# HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA ARUSHA
## MOUNT MERU

# TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA ILIYOSAMBAA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII KUHUSU HOSPITALI KUZUIA NDUGU KUCHUKUA MWILI.**

**12 Augosti, 2025 Arusha**

Mnamo 09/08/2025 majira ya saa nne na robo usiku, Hospitali ilipokea mgonjwa wa ajali aliyejulikana kwa jina la Mohamed Ally umri wa miaka 20. Mgonjwa alipokelewa na kuanza kupatiwa matibabu na ndugu zake walifika majira ya saa nane usiku baada ya kupigiwa simu ya kupewa taarifa na Hospitali.

Mgonjwa alifanyiwa uchunguzi ikiwemo kupigwa X Ray, CT Scan na Vipimo mbalimbali vya maabara. Vile vile kutokana na hali aliyokuwa nayo, alianzishiwa matibabu ya dharura na kuwekwa chini ya uangalizi maalum wa madaktari. Gharama za huduma zote zilizotolewa ziligharimu kiasi cha Shilingi. 910,000.

Ndugu wa mgonjwa walifika saa nane usiku na hali ya mgonjwa ilizidi kubadilika na kuwa mbaya pamoja na juhudi zote za kitabibu zilizokuwa zinafanywa ndani ya kitengo cha huduma za dharura ambapo ndugu walipewa taarifa.  Majira ya saa nane usiku mgonjwa alifariki dunia.

Mnamo tarehe 11/08/2025 saa mbili asubuhi ndugu wa marehemu walifika kuchukua mwili wakiongozana na marafiki wa marehemu ambao walikuwa ni vijana wa bodaboda. Ndugu walipewa bili ya gharama za matibabu na kuelekezwa utaratibu wa kulipia wakati mwili ukiandaliwa ambapo walilipa na kukabidhiwa mwili pasipo changamoto yoyote mnamo saa nne asubuhi. Aidha wakati wa kuchukua mwili vijana wa bodaboda walifanya vurugu eneo la motuari wakidai bili waliyopewa ni kubwa na isiyoeleweka.

Hospitali inatekeleza maelekezo ya Serikali ya kutokuzuia Miili ya marehemu kwa sababu ya kutokulipwa kwa bili na hivyo INAKANUSHA taarifa za upotoshaji na zenye kuleta taharuki kwamba mwili wa marehemu ulizuiliwa kuchukuliwa kutokana na bili kutokulipwa.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru inawahakikishia wananchi kuwa itaendelea kutoa huduma kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Wizara ya Afya na itaendelea kuhakikisha kila mgonjwa anapata haki ya kupatiwa huduma kwanza pasipo kikwazo chochote ikiwemo cha kukosa fedha

**Imetolewa na Ofisi ya Mganga Mfawidhi**
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha, Mt. Meru**